

**Mashirika ya jimbo, au eneo na wakandarasi wake wadogo wa Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada (SNAP, Supplemental Nutrition Assistance Program) na Mpango wa Usambazaji wa Chakula kwenye Hifadhi za Wamarekani Asili (FDPIR, Food Distribution Program on Indian Reservations) lazima wachapishe Taarifa ifuatayo ya Kutobagua:**

Kwa mujibu wa sheria ya shirikisho ya haki za kiraia na sheria na sera za haki za kiraia za Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), taasisi hii hairuhusiwi kubagua kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, jinsia (ikiwa ni pamoja na utambulisho wa kijinsia na mwelekeo wa kijinsia), imani ya kidini, ulemavu, umri, imani za kisiasa, au kulipiza kisasi kwa kuhusika katika shughuli za awali za haki za kiraia.

Maelezo ya mpango yanaweza kupatikana katika lugha zingine isipokuwa Kiingereza. Watu wenye ulemavu wanaohitaji njia mbadala za mawasiliano ili kupata maelezo ya mpango (km, Breli, maandishi makubwa, kanda ya sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani), wanapaswa kuwasiliana na shirika (la jimbo au eneo) ambako walituma maombi ya msaada. Watu ambao ni viziwi, walio na matatizo ya kusikia au walio na matatizo ya kuzungumza wanaweza kuwasiliana na USDA kupitia Huduma ya Uelekezi ya Shirikisho (Federal Relay Service) katika (800) 877-8339.

Ili kuwasilisha malalamiko ya ubaguzi katika mpango, Mlalamishi anapaswa kujaza Fomu ya AD-3027, Fomu ya Malalamiko ya Ubaguzi wa Mpango wa USDA ambayo inaweza kupatikana mtandaoni katika: <https://www.fns.usda.gov/sites/default/files/resource-files/ad3027-swahili.pdf>, au kutoka ofisi yoyote ya USDA, kwa kupiga simu (833) 620-1071, au kwa kutuma barua kwa USDA. Barua lazima ijumuishie jina, anwani, nambari ya simu ya mlalamishi, na maelezo ya maandishi ya madai ya kitendo cha ubaguzi kwa undani wa kutosha ili kumfahamisha Katibu Msaidizi wa Haki za Kiraia (ASCR) kuhusu asili na tarehe ya madai ya ukiukaji wa haki za kiraia. Fomu au barua iliyojazwa ya AD-3027 lazima iwasilishwe kwa:

- (1) **barua:**  
Food and Nutrition Service, USDA  
1320 Braddock Place, Room 334  
Alexandria, VA 22314; au
- (2) **faksi:**  
(833)-256-1665 au (202)-690-7442; au
- (3) **barua pepe:**  
[FNSCIVILRIGHTSCOMPLAINTS@usda.gov](mailto:FNSCIVILRIGHTSCOMPLAINTS@usda.gov)

Taasisi hii ni mtoa huduma asiyebagua.